# Jumbe 6 kwa Kanisa

## Muujiza wa Uponyaji na Mualiko wa Mbinguni






***Pastor: Brani Duyon***

*Utangulizi:*
*Mnamo Mei 2006, mtumishi wa Mungu alitwaliwa Mbinguni akakutana na Bwana Yesu na kupokea ufunuo wa jumbe 6. Brani Duyon @ Efendie, umri 52, ukabila wa Dusun. Ni mtumishi katika kanisa la kiinjili la Borneo, Kota Belud, Sabah (Mashariki ya Malaysia) kama Mzee wa kanisa. Aliwahi kuwa Mchungaji Melangkap Baru, Kota Belud, na baadaye akawa Kiongozi wa Kanisa SIB Bayayat kwa2005-2006.*



Mnamo Aprili 21, 2006, mke wangu na mimi tulienda Malaysia ya magharibi kuhudhuria harusi ya mtoto wetu. Kwa bahati mbaya baada ya wiki moja, niliugua ghafla kiharusi. Mara moja nilipelekwa kituo cha matibabu katika Chuo Kikuu Malaya ambapo daktari alinichunguza. Aliniambia kuwa kulikuwa na mpasuko wa seli za damu katika ubongo wangu na ilinipasa nipate upasuaji.

Nilikuwa katika comma kwa wiki moja baada ya operesheni na katika kitengo cha wagonjwa mahututi kwa mwezi 1 zaidi.

Kulikuwa na watumishi wengi wa Mungu ambao walikuja kunitembelea na kuniombea, ikiwa ni pamoja na SIB Sabah Rais wa zamani - Mchungaji Taipin Melidoi, msaidizi wake - Mchungaji Datuk Arun Selutan, na pia Mchungaji Michael.

Niliota ndoto ya mvua kubwa ikinyesha juu yangu. Nilitafsiri ndoto hii kama majibu ya maombi ya Wachungaji waliokuwa wakiniombea afya yangu. Mungu asifiwe, kwa nguvu zake nilipata nafuu mapema kuliko ilivyotarajiwa.
Usiku mmoja wa manane, wiki ya tatu ya Mei 2006, nilihisi ajabu sana. Sikuweza kwenda kulala, wakati wagonjwa wengine walikuwa wamelala fofofo. Wakati huo, nilikuwa nawaza juu ya Yesu tu.

Nalikumbuka katika Isaya 43:26 *Unikumbushe, na tuhojiane; eleza mambo yako, upate kupewa haki yako.* "Niliendelea kufikiria maneno haya kwa sababu nilitaka kuweka mawazo yangu tu juu ya Bwana Yesu. Niliweza kuhisi uwepo wa nguvu za Mungu kwa wakati huo.

Kisha nikaanza kuomba katika roho. Baada ya kuomba, nalijaribu kulala tena lakini sikuweza. Niliegemea kitanda changu. Ghafla nilihisi kana kwamba kuna mtu alikuwa ananigusa mgongo wangu na kupapasa kichwa changu. Hii iliendelea kwa muda kidogo. Nilihisi kitu kinapita/kinamiminika katika mwili wangu. Nilijua huu ulikuwa ni upendo wa baba kwa mtoto wake. Nilijiuliza mtu huyu alikuwa nani. Nilipogeuka kumuangalia, nilishangaa kuona kwamba alikuwa kijana mdogo na mzuri, amejengeka vizuri, mrefu na mwenye nywele ndefu mpaka kwenye shingo yake. Naye alikuwa amevaa mavazi meupe. Nikamuuliza, *"Je wewe ni Bwana ambaye nimekuwa nikimfikiria?"* Alitingisha tu kichwa chake. Kisha nilimuuliza tena, *"kama sio basi wewe ni nani?"* Mwisho alianza kuzungumza na mimi "*Mimi ni mjumbe kutoka Mbinguni. Yesu aliniambia nije kwako kukupa habari njema.*

Sasa nikagundua kuwa alikuwa malaika wa Mungu, hivyo nikamuuliza, *"Ni habari njema ipi unataka kuniambia?"* Akajibu, "*usiku wa leo utakwenda Mbinguni".* Mara nilijihisi shwari sana na amani ingawa mwili wangu bado ulikuwa ni mgonjwa. Nilihisi kama sikuwa na maumivu yoyote.Nilipona kabisa muda ule malaika ananiambia nitakwenda mbinguni. Kisha nikamwambia Malaika, "Niko tayari kukufuata wewe mbinguni. Siwezi kusubiri kumuona Bwana wangu. "

Tulipokuwa tukitembea niliuona mwili wangu wa duniani umebaki juu ya kitanda changu. Baada ya kutoka nje ya hospitali, nikaona farasi mkubwa na mrefu wa kushangaza. "Tutapanda farasi huyu," alisema Malaika. Malaika alinisaidia kumpanda farasi, kwa sababu alikuwa mrefu sana. Kisha nilimuuliza Malaika, *"Tunaweza kwenda Mbinguni kwa kuendesha farasi huyu?"* Malaika akanihakikishia, *"bila shaka, usiwe na hofu na wasiwasi. Umesoma Neno la Mungu kuhusu Elia ambaye alichukuliwa Mbinguni na Mungu? "*Nilimwambia*" ndiyo, nilisoma neno hilo kabla kwamba chombo kilichomchukua Elia kwenda mbinguni ilikuwa gari la moto, lililovutwa na farasi wa moto. "" Hiyo ni sawa, na huyu ni mmoja wa farasi ambaye tutampanda sasa, "*alisema Malaika. Mwanzoni tulikwenda polepole, lakini baada ya mita 100 farasi aliongeza kasi kubwa sana na nilihisi kama tulikumbwa na upepo. Kisha nikaona farasi tayari aliruka. Tulivuka milima mingi kwa urahisi, tukiruka na nguvu za Mungu.

Kisha tulifika katika eneo moja kubwa sana lenye nyasi nzuri za kijani - lilikuwa ni kamilifu, lisilo na nyasi hata moja iliyokauka. . (Zaburi 23: 2 ***"katika malisho ya majani mabichi hunilaza kando ya maji ya utulivu huniongoza"***) Baada ya farasi kusimama, tukashuka, takaanza kutembea.

Niliweza kuona Ufalme wa Mungu mbele ya macho yangu. Tulipokuwa tukitembea juu ya uwanja, nikasikia kengele inalia. Nilimuuliza Malaika "kwa nini kengele inalia?" Akasema "kengele hiyo ni ishara kwamba mtu amefika."

Tuliendelea kutembea hadi mwisho wa uwanja, wakati kengele ikiendelea kupigia. Niliona nyumba nzuri sana, juu yake kulikuwa na mwanga mwekundu, kama mwanga wa taa za trafiki. Katika mwanga huu nikaona namba "51". Naliuliza Malaika nini maana ya hii. Alisema, *"umri wako sasa ni miaka mingapi?"* Wakati huo nilikuwa na umri wa miaka 51. *"Basi namba hiyo ni umri wako, hivyo ni namba ya nyumba yako pia,"* Malaika aliniambia. Nilijisikia furaha na amani na kuona nini Mungu ameandaa kwa ajili yangu Mbinguni. Niliona nyumba nyingi ambazo tayari zimeandaliwa na Yesu kwa watoto wake walioamini na kumfuata.

Tuliendelea kutembea mpaka nyumba moja kubwa sana, yenye watu wengi ndani. Naamini hao walikuwa watu watakatifu ambao Mungu aliwachagua. Walikuwa wakimsifu Mungu. Niliona Yesu alikuwa amekaa katika kiti chake cha enzi wakati watu wote walikuwa wakimtukuza na kumuabudu Yeye. Walimsifu Yeye kwa mioyo yao yote, na kucheza, waliinyanyua mikono yao kisha wakisujudu kwa magoti yao. Ndani katika moyo wangu mimi nalisema, *"kama watu wa duniani watamsifu na kumwabudu kama hivi, Mungu atafurahishwa sana."*

Niliona watu wengi walikuwa wakilia huku wakimsifu Mungu. Yesu alitabasamu wakati anawaangalia jinsi walivyojitoa wakati wa kumwabudu Mungu. Waliinyanyua mikono yao kumuelekea Yesu na Yesu alikuwa akiwabariki wote. Baada ya huduma/ibada kumalizika, Yesu alitembea katikati yao kuwafuta machozi. Hapo nilikumbuka mstari katika kitabu cha Ufunuo, ***"hakutakuwa na kifo tena, hakutakuwa na huzuni wala kilio wala maumivu".***

Malaika akanileta kwa Yesu. Malaika alizungumza na Yesu *"Bwana, huyu ni mtoto wako ambaye Umemchagua kuja hapa."* Kisha Yesu akaniambia, ***"Ni vyema! mwanangu umekuja leo".*** Kisha Yesu akanikumbatia hii ikanifanya niwe mwenye furaha na amani kiasi kwamba nililia. Nafsi yangu iliruka kwa furaha kwa sababu Yesu mwenyewe alinikumbatia.

Malaika akasema, *"Bwana, nilikwenda nyumbani mwake duniani wakati alipokuwa mgonjwa, hata hivyo yeye sasa ni mzima."* Yesu akamjibu, ***"ndiyo, Nilisikia na kuona kilichotokea kwake."*** Malaika aliendelea, *"wakati huo, nikamsikia mke wake anaomba msaada wako. Aliomba*: ".. *Bwana, tusaidie, tafadhali usimchukue sasa kwa sababu bado hatuko tayari kwa yeye kutuacha bado" Hayo yalikuwa ni maombi yake, Bwana "*Yesu akasema***," Najua kila kitu. Mke wake ni mwanamke mcha Mungu. Yeye ni mwaminifu kwangu na mwenye bidii katika maombi."*** Nafsi yangu ililia tena ikifikiria uaminifu wa mke wangu kwa Mungu.

Kisha Mungu akasema na mimi, ***"Mwanangu, utakwenda tena Duniani, kwa sababu si muda wako bado wa wewe kuwa hapa. Kuna mengi ya kufanya wakati utakapokwenda duniani. Utakuwa na kazi sana ya kunitumikia. "***Kisha nikamjibu*," Bwana, tafadhali usinitake mimi nirudi tena duniani, kwa sababu mimi nina amani sana kubaki na wewe hapa. Najisikia furaha kuwa karibu na wewe Bwana. Tafadhali, sitaki kurudi duniani. "*

Yesu alikuwa na ujumbe kwa ajili yangu kuuleta Duniani. Yeye anilitaka mimi niwaambie ujumbe huu watoto wa Mungu walioko duniani. ***"Jumbe hizi ni muhimu sana kwa wao kujua,"*** alisema Yesu. Niliambiwa kwamba nitakuwa na kazi kubwa sana kupeleka ujumbe huu nje. Yesu pia alitaka niwaeleze uzoefu wangu wa Mbinguni watoto wote wa Mungu ili wabarikiwe na kuhuhisha nguvu zao za kumfuata.
Uso wake, nakuambia Yesu alihudhunishwa sana. Kisha nikamwomba msamaha kwa sababu nilikuwa nimemuudhi. Nikasema, *"Bwana, mimi niko tayari kwenda tena Duniani lakini tafadhali nisaidie Bwana, nipe nguvu, na uwe nami kokote nitakakokwenda. Uwe pamoja nami Bwana.* "Ndipo Yesu akasema***," ndiyo, usiwe na wasiwasi, popote utakapokwenda kunitumikia Mimi, Nitakuwa pamoja nawe daima. "***

Yesu alizungumza na mimi, ***"Utakapokwenda duniani waambie watoto wangu wote ujumbe huu"*** **(Kulikuwa na JUMBE SITA ambazo Yesu alikuwa amenipa):**

***UJUMBE WA KWANZA:***

***"Wambie Watoto wangu, ni lazima kuamini katika Mimi kwa moyo wao wote, nguvu zao, na akili zao. Wale ambao wana wasiwasi na mashaka hawatafika hapa, "****alisema Bwana Yesu***.**

***UJUMBE WA PILI:***

***"Wambie Watoto Wangu, ni lazima wawe waaminifu katika kuja kwenye ibada kanisani, kwa sababu wakati huo nitaangaza juu ya nyuso zao na wao watautazama uso wangu. Nitapendezwa sana kuona watoto wangu wakiniabudu katika Kanisa, "****alisema Bwana Yesu*

***UJUMBE WA TATU:***

***"Wambie Watoto Wangu, ni lazima wawe waaminifu kuomba, kufanya matakwa yangu, na kuishi kwa maneno yangu,"*** *alisema Bwana Yesu*

***UJUMBE WA NNE:***

***"Wambie Watoto wangu, ni lazima kuwa watiifu katika kutoa fungu la kumi na sadaka,"*** alisema Bwana Yesu.

*(Yesu alipokuwa ananipa ujumbe huu, Alisema* ***"Mtoto wangu, angalia pale"*** *Akanionyesha nyumba nzuri ambazo zilikuwa tayari kwa ajili ya watoto wake.* ***"Mwanangu, nyumba hizi ziko tayari, Nimezitayarisha kwa ajili ya watoto wangu wote wanaoamini na watiifu kwangu. "****Kisha akanionyesha nyumba zenye mapungufu. Niliuliza" Bwana, kwa nini nyumba hizi bado hazijakamilika? "Bwana Yesu alisema"* ***mwanangu, nyumba hizi ni mali ya watoto wangu ambao hutoa fungu la kumi na sadaka kwa moyo duni****(usiokunjuka).* ***Hizi nyumba zitakuwa tayari na kukamilika baada ya watoto wangu kutoa fungu la kumi zaidi na sadaka katika Nyumba yangu. "***

***UJUMBE WA TANO:***

***"Wambie Watoto wangu, ni lazima kwa maombi waweke mali zao zote kwangu kwa ajili ya ulinzi na baraka wakati wanapokuwa duniani, ili kwamba wakati nitakapokuja duniani kwa mara ya pili, hawatakuwa wameshikamana na mali zao za duniani. Kumbuka hadithi ya mke wa Lutu, "***alisema Bwana Yesu.

***UJUMBE WA SITA:***

***"Wambie Watoto wangu, ni lazima wawe tayari na tahadhari, kwa sababu mimi nitakuja hivi karibuni. Mapema kuliko watu wanavyotarajia! "***Alisema Bwana Yesu,

*(Kuja kwa Yesu hakujulikani lakini unyakuo hakika utatokea. Bwana Yesu atakuja hivi karibuni !!!)*

Wakati Yesu ananiambia ujumbe wa sita, Alinionyesha anga, ilikuwa wazi na hakukuwa na mawingu. Niliona Yesu akifungua mikono yake Duniani na Aliongea ***"Niko tayari kuchukua watoto wangu."*** Kisha nikaona watu wengi waliokuwa wamevaa nguo nyeupe wakiruka juu katika anga kukutana na Yesu. Walikuwa wamekusanyika upande wa kushoto na kulia mwa Yesu. Watu wengi ambao waliamini katika Yesu walinyakuliwa. Aidha, niliona ndugu wote wa familia nyingi walinyakuliwa. Niliwaweza kuona mume na mke na watoto wao wakiruka kumuelekea Yesu. Nilijisikia amani kuona tukio hilo.

Kisha Yesu alisisitiza, ***"angalia chini".*** Kisha Yesu alinionyesha hali ya Duniani, ilikuwa machafuko sana. Hakukuwa na amani duniani wakati huo. Niliona watu walikuwa wanakimbia kila mahali na wakipiga makelele. Wazazi walikuwa wanatafuta watoto wao na vijana walikuwa wanatafuta wazazi wao.

Yesu alinionyesha Kanisa katika mji wangu. Nilijisikia huzuni, kwa sababu kulikuwa na baadhi ya watu walioachwa nyuma.

Kisha Yesu akaniambia, ***"Uwe mwaminifu kwangu. Ni lazima ufikishe mambo yote ambayo umeona na kusikia kwa watoto wangu Duniani. "***
Kisha Malaika alinirudisha Duniani kwa farasi yule tuliyempanda kabla. Tulifika Duniani haraka sana.

Kisha Malaika akanichukua mpaka hospitali. Nilipokuwa naangalia mwili wangu wa duniani, roho yangu mara ikaingia tena kwenye mwili huo.

Niligundua mwili wangu ulikuwa umerejea afya yake nzuri. Asifiwe Mungu kwa nguvu zake!

Nakumbuka nilipokuwa Mbinguni mwili wangu ulionekana kama ulivyokuwa wakati nikiwa kijana.

Huo ni ushuhuda wangu wa kukutana na Bwana Yesu Mbinguni.



tafsiri na peter kahale